

LANDISIWALO NI MOLA

1. Landisiwalo ni mola, halifuti nguu mbili
Na halendi shela bela, aongozalo Jalali
Mafitini huliola, kwa kutaka kubadili
Wakafanya kila hila, wakashindwa kulidhili.
2. Usiku si wa kulala, ni mchana hawalali
Wakajiona ghafula, ni wakondefu miili
Si wa kunywa si wakula, kwa wivu kuwakatili
Kwa sababu Mfadhila, hazingwi kwa mizingili.
3. Zuri atowalo Mungu, mfano wa langu hili
Na lipikiwe majungu, ulozi na dawa kali
Kuomba litoke kwangu, lende kwao wakamili
Nimeshapewa na changu, nimepata kwa adili.
4. Tuzo ya bidii zangu, za juhudi na adili
Mwashikwa kizunguzungu, mwabata kwa ujuhali
Msipomokwe tiwengu, maleuni majahili
Hampoki langu fungu, pananeni kwa kitali.
5. Hivi nyinyi walimwengu, au ni majoka kweli?
Nimetuzwa kwa “upofu”, hiyo ni hoja dhahili
Au kwa hali dhaifu, kwa haya tuyajadili
Walemavu ni sufufu, nchini kila mahali.
6. Kwa ushairi arifu, alotuzwa tafadhali
“Shindano” ni hoja dufu, kutojuwa taamuli
Sema wapi bila hofu, shindano walikabili?
Tuzo ya uadilifu, kwa mabora ya awali.

(Mshairi Bora)
Amiri A. S Andanenga,
S.L.P 4775
Shariff Shamba, Dar es Salaam